



## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Benki Kuu ya Tanzania imepokea uvumi kwamba kuna zoezi la kukusanya noti mpya kutoka katika mzunguko kwa kudaiwa kuwa ubora wake ni hafifu.

Benki Kuu inapenda kukanusha habari hizi za kizushi kuwa siyo kweli na kwamba hakuna mpango kama huo.

Benki Kuu inapenda kuwahakikishia wananchi kwamba noti hizi ni bora na zinaendelea kutumika sambamba na toleo la zamani.

Kwa hiyo, wananchi waendeleo kuzipokea na kuzitumia pasipo mashaka yoyote.

Aidha, ili kuhakiki uhalali wa noti tunawashauri wananchi waendeleo kuzichunguza kwa makini noti zote wanazopokea kwa kutumia alama za usalama kama zinavyoanishwa kwenye matangazo na vipeperushi vinavyotolewa na Benki Kuu.

**Imetolewa na Idara ya Uhusiano na Umma na Itifaki**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

Machi 10, 2011